



PracticalWisdom #9

NAMNA YA KUONDOKANA NA MADENI

HATUA ⑥ RAHISI ZA KUFUATA



JOEL ARTHUR NANAUKA

Namna Ya
Kuondokana Na Madeni
Hatua 6 Rahisi Za Kufuata

Joel Arthur Nanauka

Kitabu hiki kimeandikwa na **Joel Nanauka**, Kikiwa ni kitabu cha 9 katika mfululizo wa Practical Wisdom Series.

Haki zote zimehifadhiwa. Huruhusiwi kunakili au kudurufu sehemu ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi. Kufanya hivyo itakuwa ni ukiukwaji wa haki za mwandishi na mchapaji. Ikigundulika hatua za kisheria zitachukuliwa.

Copyright 2020

Mawasiliano:

Joel Arthur Nanauka

P.O.Box 34743, Dar es salaam

Simu +255 756 094 875

Barua pepe: jnanauka@gmail.com

www.joelnanauka.com

Kimesanifiwa na Kupangwa na **Andrew Rwela**

Dar es salaam, Tanzania

0743 200 738

rwelaandrew@gmail.com

YALIYOMO

Stori Binafsi Kuhusiana Na Madeni	01
Maswali 7 Ambayo eBook Hii Inayajibu Kuhusiana Na Madeni	05
Umuhimu Wa eBook Hii Kwa Watu Wanaotaka Kutoka Kwenye Madeni	07
Dalili 4 Kubwa Ambazo Usipozijua Utashindwa Kutoka Kwenye Madeni	09
HATUA YA KWANZA: Jitathimini Hali Yako Kujua Wapi Ulikosea	14
HATUA YA PILI: Weka Vipaumbele Ujue Namna Sahihi Ya Kutoka Kwenye Madeni Uliyonayo	17
HATUA YA TATU: Mambo Muhimu Ya Kuongea Na Wadeni Wako Ili Uweze Kumaliza Madeni Yako Kwa Haraka	21
HATUA YA NNE: Maeneo 3 Ya Kuyabadilisha Haraka Ili Utoke Kwenye Madeni	27
HATUA YA TANO: Jiulize Maswali 7 Muhimu Kabla Ya Kukopa Tena Ili Usiingie Kwenye Madeni Mengine	33
HATUA YA SITA: Epuka Vifungo 6 Vikubwa Vinavyosababisha Watu Wengi Kuwa Na Madeni Yasiyoisha	40
Kuhusu Mwandishi	49

UTANGULIZI

Stori Binafsi Kuhusiana Na Madeni

Niliwahi kuwa na rafiki yangu wa karibu sana ambaye alikuwa na malengo makubwa sana ya kufanikiwa kifedha katika maisha yake.

Kutokana na ukubwa wa malengo ambayo alikuwa nayo, hakuwa mtu mwenye uoga katika kuchukua hatua. Aliamua kujiingiza kwenye biashara na ili kukuza mtaji wake alianza kukopa.

Baada ya muda alikuwa amekopa kwa watu mbalimbali na akajikuta uwezo wake wa kulipa umekuwa mdogo. Ghafla akajiingiza kwenye tabia ya kuanza kukopa kutoka kwa huyu ili akamlipe huyu. Matokeo yake, baada ya muda alizidiwa sana.

Kabla hajataka kuwa muwazi sana, nilianza kuona amepoteza furaha na mara nyingi simu yake anazima. Nilipokutana naye siku moja, niliona kabisa kuwa afya yake imedhoofika sana.

Baada ya kumlazimisha sana aongee kinachomsibu, aliniambia mambo yafuatayo:

1. Yuko kwenye madeni makubwa sana na haoni kama atakuwa na uwezo wa kuyalipa kwa sasa, amekata tamaa.
2. Madeni yamemfanya akimbie watu na aogope kwenda baadhi ya maeneo kwani anahofia atakutana na wadeni wake.
3. Mahusiano yake na mwenzi wake yameathirika sana kwani kuna madeni ambayo alimficha mwenzi wake na anaogopa kabisa kumuambia ila yanamtesa sana.
4. Amegundua kuwa uwezo wake wa kuwa mbunifu na kufikiria umepungua sana. Pia ameanza kuwa anaumwa mara kwa mara na akienda hospitali hakuna ugonjwa ambao wanaukuta.

Alipomaliza kuzungumza maneno haya, alianza kulia na kusema "Najiona sina thamani tena. Sidhani kama nitainuka tena na kutimiza ndoto yangu" Baada ya kumsikiliza, niliamua kumshawishi anipe fursa ya kumsaidia kutoka kwenye changamoto hiyo.

Tukaanza program maalumu ya kuelekea katika uhuru wa kutoka kwenye madeni. Baada ya miezi michache hali yake ikaanza kubadilika.

Hatua nilizomfundisha akazichukua na furaha ikaanza kurudi. Tulipomaliza mwaka mmoja, akajikuta kuwa amefanikiwa kumaliza madeni yake yote na anaendelea na kufukuzia ndoto yake.

Baada ya hapo aliniletea marafiki zake wenye matatizo ya madeni kama yake na nikaanza kuwasaidia pia, na wote walifanikiwa kutoka kwenye kifungo hicho.

Madeni yanatesa, yanaumiza na yanadhoofisha. Madeni yamewasababisha watu kukosa ujasiri, kuwa waongo, kujitenga na watu n.k.

Usipokuwa na maarifa maalumu ya kukusaidia kutoka kwenye madeni, unaweza kupoteza mwelekeo wa maisha yako. Madeni yameua ndoto za watu wengi sana.

Kitabu hiki kimelenga kukusaidia usiingie kwenye mtego wa madeni kama bado haujaingia huko, kama kuna madeni yanakusumbua, ujue mbinu zilizothibitishwa za namna ya kutoka.

Bila kujali hali yako ya madeni ikoje kwa sasa, amini kuwa inawezekana kabisa kutoka hapo na kuwa huru. Kama wengine waliweza kutumia mbinu hizi na kutoka kwenye madeni yao, basi na wewe unaweza pia kuzitumia na kutoka kwenye madeni yanayokukabili.

Usiamini kuwa umefika mwisho na hakuna suluhisho, sio kweli Suluhisho lipo. Utakapomaliza kusoma kitabu hiki utagundua kuwa hauko mbali sana na kupata uhuru wako kutoka kwenye kifungo cha madeni.

Karibu ujifunze elimu ambayo itakusaidia sana kupambana na changamoto ya madeni.

See You At The Top

Maswali 7 Ambayo eBook Hii Inayajibu Kuhusiana Na Madeni

Kuna watu wengi sana ambao wamekuwa wanatafuta kutoka kwenye madeni au hawatamani siku moja wajikute kwenye tatizo hili la madeni. Kupitia kitabu hiki utapata majibu ya maswali yafuatayo:

1. Hatua gani unaweza kuanza kuzichukua leo ili utoke kwenye madeni yanayokusumbua?
2. Ni makosa gani ambayo unaweza kuyaepuka ili usijikute umeingia kwenye tatizo la madeni?
3. Ni sababu zipi ambazo zinawafanya watu waingie kwenye madeni yanayowasumbua?
4. Kama madeni yameathiri afya yako, kukupa msongo wa mawazo na kupoteza furaha yako, unatakiwa kufanya nini ili urudi katika hali ya kawaida?
5. Ni aina gani ya maisha unatakiwa kuanza kuishi leo ili usisumbuliwe na madeni?

6. Kama una watu wengi sana wanaokudai hadi umeanza kuwakimbia, kuzima simu n.k unatakiwa uongee nao nini ili wakuelewe?

7. Vifungo ambavyo vimewaingiza watu kwenye matatizo ya madeni na jinsi ya kutoka.

8. Maswali 7 muhimu ya kujiuliza kabla haujakopa.

Baada ya kufika mwisho wa kitabu hiki utagundua kuwa, kutoka kwenye tatizo la madeni utahitaji kuzijua na kutumia kanuni muhimu ambazo zimethibitishwa ili ufanikiwe.

Umuhimu Wa eBook Hii Kwa Watu Wanaotaka Kutoka Kwenye Madeni.

Watu wengi sana walioko kwenye madeni wameshindwa kabisa kutoka kwa sababu wameshindwa kupata njia sahihi za kufanya.

Kuna watu ambao wameingia kwenye matatizo makubwa ya madeni na yamewasababishia msongo wa mawazo, wameharibu mahusiano, wamejiona hawana thamani tena, yameathiri afya zao, n.k.

Ukichunguza watu hawa utagundua kuwa tatizo kubwa wanalokabiliana nalo sio kwa sababu deni lao ni kubwa sana, la hasha. Bali ni kwa sababu hawakujua namna ya kukabiliana na deni lao.

Kuna watu ambao waliwahi kuwa na madeni makubwa sana na walifanikiwa kutoka katika madeni hayo na sasa wako huru. Mbinu walizotumia ndio zile ambazo zimeelezwa katika kitabu hiki, na wewe ukizitumia basi utakuwa huru kabisa.

Kwa mantiki ya kitabu hiki kuna maneno mawili muhimu kuyaelezea muktadha wa matumizi yake: MIKOPO na MADENI

MIKOPO: Ni kile unachopewa/Pesa kukiwa na makubaliano maalumu na anayekupatia ya namna utakavyolipa. Hii inahusisha MUDA wa malipo, riba itakayotumika, kiwango cha kulipa, njia za kulipa n.k.

MADENI: Ni pale unapokiuka makubaliano ya mikopo uliyowekea hapo mwanzo. Kwa mfano kama tulikubaliana kuwa utanirudishia pesa yangu baada ya wiki mbili na zikapita bila kurejesha, basi hapo mkopo niliokupatia unageuka kuwa ni deni.

Kwa mantiki ya kitabu hiki, hakikufundishi kutoka kwenye kukopa ila kinakufundisha kutoka kwenye madeni. Kama unaweza kulipa kila ulichokopa kwa wakati unaotakiwa inamaanisha haitakusumbua kabisa, ila pale unapoanza kushindwa kulipa kwa wakati hapo ndio tatizo huwa linaanzia.

Maarifa utakayoyapata kwenye kitabu hiki, yatakusaidia sana kujiepusha na kuwa katika madeni ambayo yanaweza kuathiri sana mafanikio yako.

SEHEMU YA KWANZA

Dalili 4 Kubwa Ambazo Usipozijua Utashindwa Kutoka Kwenye Madeni.



SEHEMU YA KWANZA

Dalili Za Kuzianguzia Mapema Kuhusu Madeni.

Kila siku kuna watu ambao wanatoka kwenye kitanzi cha madeni, wengine ndio wanaingia na wengine wasipokuwa makini wataingia hivi karibuni.

Watu wengi sana huwa wanajikuta kwenye madeni makubwa na mabaya bila wao wenyewe kujitambua. Inawezekana hata wewe hukuwahi kufikiria kuwa utajikuta ukiwa kwenye madeni makubwa yanayokusumbua namna hii.

Hata hivyo kuna dalili ambazo unaweza kuzianguzia kujua kuwa tatizo la madeni linakunyemelea au limeshakukamata tayari.

Baadhi ya dalili hizo ni pamoja na:

1. Unakopa Kwaajili Ya Mahitaji Muhimu.

Yaani kama wewe kila siku unakopa kwaajili ya "kusurvive", yaani mahitaji muhimu ili maisha yaendeleo, inamaanisha uko tayari kwenye mtego wa kuingia kwenye madeni.

SEHEMU YA KWANZA

Kama wewe kila wakai unakopa pesa ya chakula, kodi ya nyumba, ada za watoto za shule n.k hii inamaanisha tatizo la madeni limeshakukamata na kuna hatari ukashindwa kabisa kutoka hapo baadaye.

Hebu jikague leo, wewe ni mmoja wa watu wenye hii dalili kwa sasa? Kila inapofika wakati wa kulipa mahitaji muhimu basi ni lazima ukope.

2. Kipato Chako Hakitoshi Kwa Mwezi Husika.

Kila wakati unapopata mshahara wa mwezi huwa hauwezi kufika tarehe ya mwisho wa mwezi, unaishia njiani. Yaani kila unachopata kwa mwezi husika huwa kinatosha kwa siku kadhaa tu, pengine wiki mbili tu za mwezi na baada ya hapo inabidi uanze kukopa ili kumaliza mwezi.

Wakati mwingine, hata kabla haujapata pesa mkononi kwa mwezi husika, tayari unajikuta umeshazimaliza kabla haujazitumia kwa sababu ya madeni husika.

Kama ukiona kuwa kipato chako cha mwezi husika hakikidhi mahitaji yako inamaanisha wewe uko kwenye

SEHEMU YA KWANZA

orodha ya watu ambao madeni yatawasumbua sana.

3. Unakopa Ili Kulipa Madeni.

Umeshaingia kwenye ile staili ya maisha ya kukopa hapa ili ulipe pale. Yaani, unafukua shimo hapa ili ukafukie sehemu nyingine. Hii inamaanisha kuwa, hakuna siku ambayo utakuwa umeshatoka hapo, kwa sababu kila siku unakopa sehemu moja ili ukalipe sehemu nyingine.

Ukishaona kuwa mikopo yako wewe sio kwa ajili ya kufanya shughuli fulani ya maendeleo au uwekezaji, ila ni kwa ajili ya kulipa deni mahali pengine, inamaanisha kuwa umeshaingia kwenye tatizo hili na lazima uangalie namna ya kulishughulikia mapema kabla halijawa mzigo mkubwa sana kwako.

4. Umeanza Kuwakimbia Wanaokudai.

Ukianza kuona unawakimbia wanaokudai kwa kuwakwepa ukiwaona unabadilisha njia, unazima simu au unabadilisha namba mara kwa mara ili kuwakwepa, unawadanganya kuwa umesafiri, unaanza kukwepa kwenda baadhi ya maeneo ili usije ukakutana nao n.k.

SEHEMU YA KWANZA

Hii inaonyesha kuwa tayari kuna tatizo limeshaingia kwenye maisha yako. Hata kama haujakiri kuwa uko kwenye tatizo la madeni ila ukweli ni kuwa utakuwa tayari umeshakamatwa na changamoto hii tayari.

Je, wewe ukijitafakari unaona kuna dalili yoyote kati ya hizi ambazo unazo?

SEHEMU YA PILI

HATUA YA KWANZA: Jitathimini Hali Yako Kujua Wapi Ulikosea



SEHEMU YA PILI

Ili kutoka kwenye madeni kuna hatua ambazo lazima uzifuate ili utoke salama. Watu wengi sana baada ya kujikuta kwenye madeni, huwa hawajui wafanye nini na matokeo yake huwa wanabakia katika tatizo hilo kwa muda mrefu sana.

Kama leo umeziona dalili za kuwa kwenye madeni mabaya, kuna hatua ambazo unaweza kuanza kuzichukua haraka:

Hatua ya kwanza kabisa ni - **JITATHMINI HALI YAKO** (Know Your Status)

Kuna watu wengi sana ambao wako kwenye madeni lakini hawajui hali yao ya sasa. Kabla haujaanza kutaka kutoka kwenye madeni, jua ukubwa wa changamoto inayokukabili.

Jiulize maswali yafuatayo:

1. Nani anakudai?
2. Kila Mtu anakudai kiasi gani?

SEHEMU YA PILI

3. Makubaliano ya kulipa yakoje?

Maswali haya yatakusaidia kujua ukubwa wa tatizo ulilionalo ili utakapoanza kulipa iwe ni rahisi sana.

Hebu jaribu kufanya zoezi hili kwa sasa kabla haujaendelea hatua ya pili.

SEHEMU YA TATU

HATUA YA PILI: Weka Vipaumbele Ili Ujue Namna Sahihi Ya Kutoka Kwenye Madeni Uliyonayo



SEHEMU YA TATU

Mara baada ya kujua ukubwa wa deni ulilionalo, kinachofuata ni kutengeneza kipaumbele cha namna unavyoweza kulipa deni hilo. Kumbuka ulipokuwa unafanya tathmini ilikusaidia kujua aina mbalimbali za madeni na jinsi yalivyo.

Katika hatua hii unachofanya ni kuweka vipaumbele vya namna ya kulipa deni hilo.

Vipaumbele vyako vya kulipa deni unaangalia mambo makubwa yafuatayo:

1. Riba / Interest

Hapa kigezo unachotumia ni kuangalia yale madeni ambayo kadiri unavyochelewa kulipa, basi riba yake inazidi kuongezeka kila siku kwa kasi sana. Kuna watu wengi sana ambao leo wanakabiliwa na madeni ambayo wanachodaiwa ni mara tatu ya walichokopa kwa sababu waliacha kulipa kwa wakati na riba ikaongezeka.

2. Madhara ya kihisia / Emotional Impact

Kuna madeni ambayo yanaweza kuwa ni madogo sana na riba yake ni ndogo ila changamoto ikawa ni kwenye

SEHEMU YA TATU

madhara ya kihisia.

Unapoweka vipaumbele vya kulipa madeni yako, unaangalia pia madhara ya kihisia yanayoweza kutokana na deni ulilonalo. Kuna madeni yanaweza kuwa madogo sana ila yakakugombanisha na watu muhimu, yakakufanya ukose amani kabisa n.k.

3. Ukubwa wa madhara ya kutokulipa / Kuchelewa kulipa

Kitu kingine unachoweza kukitumia kwenye kuweka vipaumbele vya kulipa madeni yako ni kuangalia madhara makubwa yanayotokea kama utachelewa kulipa au hautalipa kabisa. Kila deni linatofautiana katika ukubwa wa madhara yake.

Kuna madeni yatapelekea kuuzwa nyumba yako, gari lako, kiwanja n.k hivyo ni muhimu sana kuangalia kila deni na kujua ukubwa wa madhara ya kuchelewa kulipa/kutokulipa kabisa.

Vigezo hivi ndivyo unatakiwa kuvitumia kuangalia vipaumbele vya deni lipi lianze kulipwa na lipi lisubirie.

SEHEMU YA TATU

Jaribu sasa kupitia orodha ya madeni yako na uangalie namna ya kuweka vipaumbele vya jinsi ya kulipa.

SEHEMU YA NNE

HATUA YA TATU: **Mambo 3 Muhimu Ya Kuongea Na** **Wadeni Wako Ili Uweze Kumaliza** **Madeni Yako Kwa Haraka**



SEHEMU YA NNE

Baada ya kuweza kujua ukubwa wa madeni uliyonayo na kuweka kipaumbele cha namna ya kulipa. Hatua ya muhimu sana ni kuzungumza na wadeni wako.

Watu wengi sana huwa wanafanya kosa la kuwakimbia wadeni wao kwa kuamini kuwa kwa kufanya hivyo wanatatua tatizo bila kujua kuwa wanazidi kutengeneza tatizo kubwa.

Inawezekana mtu anayekudai ni mkali sana, huwa ana maneno ya hovy na ana hasira sana. Na wewe unajiambia "Nitamkimbia hadi siku ambayo nitapata ndio nitamtafuta".

Hii sio fikra sahihi, kwani kadri ambavyo unamkimbia, haupokei simu yake, unamkwepa n.k ndivyo unavyozidi kumpandisha hasira.

Lazima umkabili mdeni wako!

Ukishaweka mpango wako maalumu wa kulipa madeni, unatakiwa uweke mpango wa kuongea na wadeni wako. Mambo muhimu unayoweza kuongea nao ni haya

SEHEMU YA NNE

yafuatayo:

1. Kupunguza/ Kusitisha Riba

Usiogope kufanya mazungumzo na wadeni wako kwa kuwaomba kuhusu kupunguza riba ya deni lako. Kuna wengi ambao wakijua kuwa uko serious na kulipa deni, watakuwa tayari kupunguza riba wanayokudai.

Kwa upande mwingine unaweza kuwaomba kuwa riba wanayokudai isitishwe ili upate uwezo wa kulipa deni lote la nyuma, kwa kuwaonyesha mpango wako wa namna unavyotaka kulipa deni hilo.

Kwa uzoefu wangu nimegundua kuwa watu wengi wako tayari kulegeza masharti kama wakiona kweli mtu amedhamiria kulipa. Badala ya kusema kuwa watakataa, amua kuchukua hatua leo kufanya hivyo.

2. Kuongeza Muda Wa Malipo / Debt Restructuring

Kwa upande mwingine unaweza kuomba kuongezewa muda wa malipo ya deni lako. Hii ni kwa ajili ya kutengeneza muda zaidi wa kujenga uwezo wa kupata pesa za kulipa.

SEHEMU YA NNE

Kama deni lako linatakiwa kulipwa kila mwezi unaweza kuomba kuwa unaruka mwezi mmoja mmoja. Hii ni kukusaidia kutengeneza uwezo wa kujikusanya zaidi.

Au unaweza kuomba kama imebaki miezi 6 unayotakiwa kumaliza deni lako, ukaomba kuongezewa miezi zaidi bila kuongezewe riba. Hata taasisi za fedha huwa zinakubali mazungumzo ya namna hii.

Ingawa itaongeza kiwango cha pesa utakachotakiwa kulipa ila ni njia nzuri ya kupunguza mzigo unaotakiwa kuubeba kila mwezi na itakupa nafasi ya kukusanya nguvu zaidi.

Kumbuka mazungumzo haya yote yanalenga kukusaidia kupata muda wa kujipanga zaidi.

3. Usitoe Ahadi Unayojua Hauwezi Kuitimiza

Watu wengi sana huwa wanadhani njia nzuri ya kunyamazisha wadeni wao ni kuwadanganya. Matokeo yake, kila siku huwa wanaamua kutoa ahadi ambazo wanajua kabisa hawawezi kuzitimiza kwa wakati, ila wanafanya hivyo ili tu kuwanyamazisha wadeni wao.

SEHEMU YA NNE

Matokeo yake, wanazidi kuwakasirisha wadeni wao kwa sababu wanaona hawako serious na kulipa. Siku zote anayekudai atakuheshimu kama unatoa ahadi unazoweza kuzitimiza.

Kumbuka kuwa, mtu anayekudai atachukia zaidi pale atakapogundua kuwa ulimdanganya kuliko atakavyochukia utakayomwambia ukweli kuwa hauwezi kulipa kwa wakati ambao anautaka yeye.

Kitu cha muhimu hapa, ni kila wakati hakikisha wewe ndio unawatafuta wanaokudai kabla hawajakutafuta. Hata kama haujaweza kutimiza ahadi mliyokubaliana, iwe ni kawaida yako kufanya hivyo.

Hii inasaidia kuonyesha kuwa uko "serious" na kulipa deni unalodaiwa. Ukiwa unasubiri hadi anayekudai akutafute inaanza kumuudhi, kumtia hasira na kumuonyesha kuwa hauna nia ya dhati kulipa deni lake.

Hii inaweza kupelekea kuwa mkali zaidi na kuchukua hatua ambazo zitakuathiri. Hakikisha wewe ndiye unampa

SEHEMU YA NNE

"updates" mdeni wako mara kwa mara kuliko yeye kukutafuta kila wakati.

Wakati mwingine ili kumfanya mdeni wako aone kuwa unamaanisha unachosema, inawezekana ukalazimika kwenda kumuonyesha mpango ulionao kwa maandishi kabisa. Utafanya hivi pale unapoona ina ulazima.

Tafakari:

Kwa kuangalia watu wanaokudai kwa sasa, unadhani ni mambo gani ambayo unatakiwa kuongea na wadeni wako?

SEHEMU YA TANO

HATUA YA NNE: **Maeneo 3 Ya Kuyabadilisha** **Haraka Ili Utoke Kwenye Madeni**



SEHEMU YA TANO

Ili upate uwezo wa kulipa madeni yako, ni lazima ufanye mabadiliko ya haraka sana. Kuna maeneo matatu ambayo unatakiwa kuyazingatia:

Eneo La Kwanza: Kubadilisha Bajeti Yako

Huwezi kupata uwezo wa kulipa madeni yako bila kufanya mabadiliko muhimu ya kibajeti. Katika kozi ya madeni ambayo unaweza kujiunga pia huwa tunafanya zoezi la 50/30/20 kama sehemu ya kubadilisha bajeti.

Ili uweze kulipa madeni yako ni lazima upunguze baadhi ya matumizi yasiyo ya lazima. Jaribu kuangalia maeneo ambayo unajua kabisa kuwa ukiyapunguza hayatakuwa na madhara ili pesa unayopata uipeleke kwenye kulipa madeni.

Baadhi ya vitu unavyoweza kupunguza ni pamoja na:

- a). Manunuzi ya nguo
- b). Kula sehemu za bei ghali
- c). Matumizi ya bundle za kupiga simu na internet

SEHEMU YA TANO

d). Michango ya makundi mbalimbali n.k

Leo jaribu kupitia bajeti yako ya mwezi na uangalie maeneo ambayo unatakiwa kuyapunguza ili upate uwezo wa kulipa madeni.

Kama haujawahi kabisa kuwa na bajeti inayoongoza maisha yako basi ni muhimu sana kufanya hivyo ili kuhakikisha kuwa unatoka kwenye changamoto hii, USIONE UVIVU, CHUKUA HATUA.

Eneo la Pili: Tafuta Namna Ya Kuongeza Kipato Chako.

Kitu cha pili na cha muhimu sana cha kuzingatia ni kuhakikisha kuwa unaweka mikakati ya kuongeza kipato chako. Mbinu ya kupunguza kipato chako ni ya upande mmoja ila lazima upande wa pili uangalie namna ya kuongeza kipato chako.

Kipato chako kinaweza kuongezeka kwa mbinu zifuatazo:

a). Kwa kutafuta kitu cha ziada cha kufanya zaidi ya unachofanya sasa hivi. Je, unaweza kupata kazi ya ziada

SEHEMU YA TANO

ukiaha unayofanya sasa hivi? Kumbuka hii inaweza isiwe kitu cha kufanya siku zote ila ni kitu muhimu ili kukutoa kwenye madeni.

b). Kuweka mikakati ya kupanua uanchofanya sasa hivi ili uongeze pesa zaidi. Hii inaweza kuwa ni pamoja na kuzalisha zaidi au kufikia wateja wengi zaidi.

Je, katika hichohicho unachofanya sasa hivi, unawezaje kukifanya kwa ukubwa zaidi ili kipato chako kiongezeke?

c). Unaweza kuamua kutafuta ujuzi zaidi ili ukupe uwanja mpana zaidi wa kufanya mambo. Jaribu, kuangalia kama ukiongeza ujuzi zaidi ulionao katika eneo lako utasaidia kuongeza kipato chako.

Au, unaweza kuamua kutafuta ujuzi tofauti kabisa na ulionao sasa hivi na ukakusaidia kuongeza kipato chako.

Je, wewe katika maeneo haya matatu ya kuongeza kipato chako unaona njia ipi ndio nzuri zaidi kwako kwa sasa?

SEHEMU YA TANO

Eneo La Tatu: Unaweza Kuuza Baadhi Ya Vitu.

Kumbuka kuwa mbinu hizi za kutoka kwenye madeni zinalenga kukuweka kuwa huru kutoka kwenye changamoto hii ili uishi maisha ya furaha.

Unaweza kuangalia katika vitu unavyovimiliki, ni vitu gani ambavyo unaweza kuamua kuviuza kwa sasa kama sehemu ya kukuweka huru na madeni.

Kumbuka, unapouza haimaanishi hautanunua tena, ila inamaanisha kwa wakati huu umuhimu wa kuwa huru kutoka kwenye deni ni mkubwa kuliko kumiliki hicho kitu.

Inawezekana kuna baadhi ya watu hawatakuelewa na watakucheka, ila kama wewe umeweka mpango wako vizuri wa kutoka kwenye kifungo cha madeni, basi chukua hatua.

Inawezekana kuwa ni simu yako, shamba, gari , n.k.. Wewe mwenyewe ndiye unatakiwa kuamua ili utoke haraka kwenye tatizo linalokukabili.

SEHEMU YA TANO

Je, wewe kuna kitu gani unaona unaweza kukiuzua kama sehemu ya kutoka kwenye madeni yako? Ukishatulia hapo baadaye unaweza kuja kukinunua tena.

SEHEMU YA SITA

**HATUA YA TANO:
Jiulize Maswali 7 Muhimu Kabla
Ya Kukopa Tena Ili Usiingie
Kwenye Madeni Mengine.**



SEHEMU YA SITA

Baada ya kujua mbinu zote hizi ni muhimu kujua kuwa, kuna wakati utahitaji kukopa pesa mahali kwa kitu fulani. Kama nilivyotangulia kusema hapo awali, suala la kukopa sio baya kama una maarifa muhimu yanayotakiwa.

Hata hivyo kuna mambo ya msingi ya kuzingatia kabla haujachukua mkopo wowote ule ili usigeuke kuwa ni deni.

Kila wakati kabla haujakopa, jiulize maswali haya:

1. Je, ni lazima nikope kwa sasa?

Kuna mara nyingi watu wanakopa tu kwa sababu kuna fursa ya kufanya hivyo. Kwa sababu yuko kwenye VICOBA au ametembelewa na afisa wa Benki basi anaamua kukopa. Kumbuka kuwa, haimaanishi kwa sababu una fursa ya kukopa basi ukope tu, hapana.

Jiulize - Hivi kweli kuna umuhimu wa kukopa kwa sasa. Kanuni nzuri huwa inasema-"Mara unapojiona unahitaji kukopa, jilazimishe kughairisha angalau kwa wiki moja.

Kama bado utaona umuhimu upo basi inawezekana mkopo

SEHEMU YA SITA

huo ni muhimu. Kama umuhimu hakuna basi achana nao.

2. Ninahitaji kiasi gani?

Kabla haujakopa, piga mahesabu kamili utahitaji kiasi gani cha mkopo. Kumbuka siku zote wakopeshaji watataka kukukopesha zaidi ya unavyohitaji, usikubali.

Ukichukua zaidi ya pesa unayohitaji, siku zote ile iliyozidi utaitumia vibaya. Kabla haujakopa piga bajeti na upate kiwango kamili unachokihitaji na usizidishe.

3. Umeshaweka bajeti ya matumizi ya mkopo wako?

Ni hatari sana kuchukua mkopo bila kujua utautumiaje. Kabla pesa hazijafika mkononi mwako au kuingia kwenye akaunti yako, hakikisha kuwa na bajeti iliyoandikwa vizuri ambayo inaonyesha kila pesa ya mkopo itaenda wapi.

Ni hatari sana kuanza kutumia pesa ya mkopo bila kuwa na bajeti iliyoandikwa. Hapa ndio utakuta mtu anaanza kutumia pesa ya mkopo wa biashara kuchangia harusi.

Kumbuka kuwa pesa ya mkopo mara nyingi unapoipata

SEHEMU YA SITA

inaonekana nyingi, hadi itakapoanza kuisha na kuanza kudaiwa ndio akili huwa inarudi. Panga matumizi yake kabla haujashika mkononi mwako.

4. Umeshajua utalipaje?

Waswahili husema "Kukopa Sherehe, kulipa Majanga". Kabla haujachukua mkopo ni muhimu sana kujua namna utakavyolipa mkopo wako. Utaulipa kupitia mshahara wako? Utaulipa kupitia faida ya biashara n.k

Kumbuka mbinu na njia za kulipa mkopo huwa hazitafutwi baada ya kuutumia. Huwa zinatafutwa kabla haujaanza kuutumia.

Kabla haujachukua mkopo, hakikisha umeandika vizuri namna utakavyolipa.

5. Umejua vizuri vigezo na masharti?

Watu wengi sana niliokutana nao na wameingia kwenye madeni mabaya, utasikia wanasema "Yaani sikujua kama masharti ndio yako hivi".

SEHEMU YA SITA

Mara nyingi watu wengi wanapokopa kwa sababu wanakuwa na shida huwa hawajipi muda kufuatilia vigezo vyote. Na mara nyingi wakopeshaji huwa hawaweki wazi vigezo fulani kwani usipovitimiza kwao ni faida kubwa.

Unapochukua mkopo usikubali kusaini kitu ambacho haujakisoma ama haujakielewa. Usikubali kuharakishwa kwani katika kufanya hivyo unaweza kukubali kitu ambacho baadaye kikawa mtego mkubwa sana utakaokusumbua.

Baadhi ya mambo ya msingi ya kuyaangalia; ni pamoja na:

- Riba italipwa kiasi gani?
- Unahitaji dhamana gani?
- Ukichelewa kulipa mkataba unasemaje? (Riba inaongezeka? unauziwa vitu? unapelekwa polisi n.k)
- Ukishindwa kulipa hatua gani zinachukuliwa?

SEHEMU YA SITA

6. Je, ni lazima nikope kwenye taasisi?

Inawezekana umeona ni muhimu sana kukopa, Je ni lazima ukakope kwenye taasisi?

Kuna uwezekano wa kukopa kwa ndugu, rafiki au jamaa ambako masharti ni nafuu zaidi ukilinganisha na kwenye taasisi?

7. Una mtu wa kukusaidia nidhamu yako ya fedha?

Watu wengi sana huwa hawana kabisa nidhamu inapofika kwenye suala la pesa. Hii ndio maana akishapata pesa tu huwa anazitumia zote tena hovy hovy.

Ili kuepukana na jambo hili nakushauri, tafuta mtu ambaye atakusaidia kusimamia nidhamu yako ya pesa. Mtu huyu unamshirikisha kabla haujachukua pesa za mkopo ili akushauri kuona kama kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

Kama umuhimu utaonekana, utampatia pia bajeti yako ya utakavyotumia mkopo wako na namna utakavyoulipa. Ila pia, hakikisha unamshirikisha kila ambapo unatumia zile pesa zako za mkopo. Hii itakusaidia kuwajibika.

SEHEMU YA SITA

Kumbuka jambo hili: Sio kila unapokuwa na tatizo basi unakimbilia kukopa, hakikisha umejiuliza maswali haya kabla haujaenda kukopa tena.

SEHEMU YA SABA

HATUA YA SITA:
Epuka Vifungo 6 Vikubwa
Vinavyosababisha Watu Wengi
Kuwa Na Madeni Yasiyoisha



SEHEMU YA SABA

Kuna baadhi ya watu kitu ambacho kimewasababisha wawe kwenye madeni yasiyoisha ni vifungo ambavyo vinaendesha maisha yao.

Kuna viu vinaendelea kwenye maisha yao na vimewakamata katika namna ambayo wanashindwa kabisa kusogea hatua mbele.

Pamoja na yote ambayo wamejifunza hadi kufikia sasa, tabia hizi zimeuwa chanzo cha wao kutofanikiwa kutoka kwenye madeni na kujikuta kila baada ya muda wanarudi tena walikotoka.

1. Kuzoea Madeni.

Kuna watu ambao wameamua kuyazoea madeni na wanaamini kuwa haiwezekani kuishi bila madeni. Watu hawa utawasikia wanasema misemo kama "Madeni hayaui" au "Hata mabilionea wanadaiwa" n.k. Wengi wanatumia maneno haya kuhalalisha kifungo chao.

Hakuna mtu anayefurahia kuwa na madeni duniani, hivyo kama yatatokea kwako basi yanatakiwa yawe ni yale

SEHEMU YA SABA

ambayo umeshindwa kabisa kuyakwepa. Tabia ya kuzoea madeni imewafanya watu wawe wanakopa hovyohovyoy bila nidhamu.

Inawezekana bado hayajakudhuru, ila madeni ukiyazoea sana yanaweza kukupa madhara ambayo haujayatarajia. Usikubali kuzoea madeni na uwe na mpango wa kujitoa kwenye madeni na kuyashinda kabisa.

2. Ulevi Wa Pombe.

Kuna watu ambao changamoto kubwa sana ya madeni waliyonayo ni kwa sababu ya ulevi wa pombe. Watu hawa kila pesa wanayopata huwa wanaielekeza katika unywaji wa pombe, matokeo yake wanapoteza kila kipato wanachopata.

Wakishamaliza walichonacho kinachofuata ni kwenda kukopa ili wapate pesa za kunywa tena.

Kama wewe ni mmoja mwenye tatizo hili unatakiwa kubadilisha marafiki na maeneo unayotembelea. Ila kama unaona tatizo hili ni kubwa sana, pengine utahitaji msaada

SEHEMU YA SABA

wa kisaikolojia au msaada wa kiroho, usipuuzie, tafuta msaada.

3. Ulevi Wa Kununua Vitu (Shopaholic)

Yako madeni yanayosababishwa na watu kuwa na ulevi wa kununua vitu hata ambavyo hawavihitaji. Yaani kuna watu wakipata pesa ni kama inawawasha, kila kinachopita mbele yao huwa wanataka kununua na mwisho wa siku wanajikuta wameishiwa kabisa.

Watu wa namna hii akili yao huwa inarudi baada ya kumaliza kila walichonacho au pesa yao inapobakia kidogo sana.

Kama wewe ni mmoja wa wale wenye tatizo hili unatakiwa kujenga nidhamu ya pesa, nakushauri tafuta kitabu changu cha **MONEY FORMULA** (Kwa lugha ya kiswahili) ambacho kinafundisha elimu ya fedha isiyofundishwa shuleni na kitabu changu kinachoitwa **ONGEZA KIPATO CHAKO**, vitakusaidia sana.

SEHEMU YA SABA

4. Chakula

Kuna watu wengine tatizo kubwa walilionalo ni kupenda kula kusikokuwa na nidhamu. Yaani akipata pesa, atanza kuzunguka kila mgahawa na kila mahali akila vitu mbalimbali.

Watu wa namna hii kama wako kwenye familia, huwa wakiwa na pesa wananunua kila aina ya chakula na wanapika kwa wingi hadi vinabaki. Akili ya kuweka bajeti huwa inarudi pesa zinapoanza kuisha.

Njia nzuri ya kukabiliana na hili ni kutumia bajeti ya 50/30/20 kama nilivyoielezea katika kitabu cha **MONEY FORMULA**.

5. Kushindwa Kusema Hapana

Kifungo cha kushindwa kusema hapana, kimewaingiza watu wengi sana kwenye madeni. Kuna watu wengi ambao wanaingia kwenye madeni kwa sababu ya hofu ya kuwaambia watu hapana.

Watu wa namna hii wanajikuta wanalazimishwa kukopa vitu

SEHEMU YA SABA

ambavyo wanajua hawana pesa za kulipa. Wanalazimishwa kuahidi michango ambayo wanajua hawataweza kulipwa n.k.

Kama unataka usiingie kwenye tatizo la madeni lazima ujifunze kusema hapana bila uoga wala hofu yoyote ile. Kumbuka hauwezi kumridhisha kila mtu kipesa.

6. Kuishi Juu Ya Kipato Chako

Kuna watu ambao wanaingia kwenye madeni kwa sababu wanajaribu kuishi juu ya kipato chao.

Yaani watu hawa huwa wana tatizo la kutaka kuonyesha wengine kuwa wamefanikiwa tayari au wameshafika level fulani ya maisha ambayo kiuhalisia bado hawajafika.

Kwa sababu ya kifungo hiki huwa wanajikuta wanaishi nyumba za gharama kubwa kuliko uwezo wao, wanapeleka watoto shule za gharama kubwa sana, wananunua nguo za gharama kubwa sana n.k.

Hii inasababisha kila wakati wajikute wakiwa na kipato

SEHEMU YA SABA

kidogo kuliko wanavyoweza kutimiza wajibu wao wa kifedha.

Usikubali kuwa katika kundi la watu ambao kila wakati wanajaribu kuwa juu ya uwezo wao. Ishi kwa kiwango ulichopo na wakati wako ukifika wa kuwa juu zaidi basi utafika tu.

Ukishagundua hii ndio imekuwa sababu kubwa, unaweza kuchukua hatua za kurekebisha aina ya maisha unayoishi kwa kutafuta nyumba ya gharama ndogo zaidi, kununua simu ya gharama ndogo, kupunguza gharama zako za nguo, kutokwenda sehemu za starehe n.k.

Tafakari:

Je, kuna kifungo chochote kati ya hivi ambacho unaona kimekuwa chanzo cha madeni kwenye maisha yako?

Nini Kinafuata Baada Ya Hatua Hizi?

Hongera sana kwa kujifunza hatua hizi zote.

Baada ya mambo haya yote epuka makosa yafuatayo ambayo yamesababisha watu wengi sana washindwe kutoka kwenye madeni.

1. Kuna watu hawachukui hatua kama ilivyoelekezwa. Hawatathimini madeni yao, hawaweki vipaumbele na wanaogopa kuongea na wadeni wao. Ukiwa mmoja wa watu wa namna hii basi hautatoka kwenye madeni

2. Kuna ambao huwa wanaamini deni lao litaishia tu hewani baada ya kukaa kwa muda mrefu. Kuna wengine wanaamini watasamehewa kimiujiza na kuna wengine wanaamini wanaowadai watasahau siku moja.

3. Kikwazo kingine ni pale mtu anapoogopa kubadilisha mfumo wake wa maisha. Anataka aendelee kuishi kama zamani. Hataki kubadilika kupunguza matumizi yake na hataki kuonekana kuwa wa tofauti.

Wewe chukua hatua leo kuanza kukabiliana na wadeni wako

ili uwe kama wale wengine waliofanikiwa kutoka kwenye madeni.

Nakutakia mafanikio makubwa.

KUHUSU MWANDISHI



Joel Arthur Nanauka,

Joel Arthur Nanauka ni mwalimu anayefundisha sayansi ya maisha, kijana mwenye ushawishi mkubwa juu ya maendeleo kibinafsi, mkufunzi wa mashirika na mwandishi wa vitabu 20 vya Kiswahili, Kiingereza na Kifaransa.

KUHUSU MWANDISHI

Joel alichaguliwa kutoa mafunzo ya mwaka mmoja kwa vijana wajasiriamali wanaowania tuzo zilizoandaliwa na Benki ya BMCE iliyopo Casablanca Morocco.

Mwaka 2019, Joel alitambuliwa na Avance Media iliyoko Ghana, kama kijana wa Kitanzania mwenye ushawishi mkubwa kwenye eneo la maendeleo binafsi na taaluma (Personal development and Academia) na alitajwa kwenye nafasi ya saba kama kijana mwenye ushawishi zaidi nchini Tanzania kwa ujumla.

Joel pia aliwahi kutajwa na Mkutano wa kimataifa wa uongozi wa vijana kama kiongozi bora wa vijana ulimwenguni nchini Taiwan-China mnamo mwaka 2002. Anatambuliwa na Graca Machel Trust (GMT) kama mshauri wa biashara kwa wanawake wajasiriamali.

Mwaka 2019, Joel alikuwa mshauri mkuu wa biashara na usimamizi katika kufanya mabadiliko kwenye vituo vikuu 6 vya habari nchini Tanzania akivisaidia kufuata mfumo ulio bora wa ujasiriamali.

KUHUSU MWANDISHI

Mwaka 2018 alichaguliwa na Baraza la kitaifa la uwezeshaji wananchi kiuchumi (National Economic Empowerment Council) lililo chini ya ofisi ya Waziri Mkuu kuwa kwenye kamati ya ufundi ya kuandaa mwongozo wa mafunzo ya ujasiriamali kwa ajili ya biashara ndogo ndogo, za kati na kubwa.

Joel amepata elimu yake rasmi kwenye mambo ya usimamizi wa biashara (Bcom), maendeleo ya kimataifa, usimamizi wa miradi, uongozi na Diplomasia ya Uchumi na pia alishawahi kufanya kazi na Shirika la Umoja wa Mataifa (UNESCO) katika programu ya kimkakati kwenye sekta ya Elimu.

Joel anajulikana kwa kutoa mafunzo yenye matokeo chanya katika mashirika ya kimataifa, mashirika ya kitaifa na mashirika muhimu ya serikali katika maeneo ya uongozi, usimamizi, biashara na utendaji wa kiwango cha juu sana.

Joel alikuwa mwanafunzi bora kitaifa kwenye mtihamu wake wa kidato cha nne na mwanafunzi bora katika masomo yake baada ya kuhitimu Diplomasia ya Uchumi (Post-Graduate Studies in Economic Diplomacy).

KUHUSU MWANDISHI

Joel anaongoza kampuni inayotoa mafunzo mbalimbali ya Africa Success Academy (ASA) yenye ofisi zake jijini Dar es Salaam nchini Tanzania. Joel amemuoa Rachel na wamebarikiwa kuwa na watoto wawili wa kike, Joyous and Joyceline.

VITABU VINGINE VILIVYOANDIKA NA JOEL ARTHUR NANAUKA

HARDCOPY (*Nakala ngumu*)

1. Timiza Malengo Yako (Mbinu 60 walizotumia watu maarufu kufanikiwa)
2. Ishi Ndoto Yako (Siku 30 za kuishi maisha unayotamani)
3. Tabia 12 Zinazoleta Mafanikio.
4. Ishinde Tabia Ya Kughairisha Mambo.
5. Ongeza Kipato Chako (Maarifa juu ya fedha, Biashara na uwekezaji)
6. Nguvu Ya Mwanamke.
7. Mbinu Za Kufanikisha Ndoto Katikati Ya Changamoto.
8. How To Pass Your Exams With Ease.
9. Uzalendo Na Ujenzi Wa Taifa.
10. Ufanisi Kazini.
11. Boresha Mahusiano Yako.

SOFTCOPY (*Nakala laini*).

1. Money Formula (Elimu ya fedha isiyofundishwa shuleni)
2. Hatua Sita Za Kujiajiri
3. Muongozo Wa Mafanikio
4. Core Genius (Jinsi ya kugundua uwezo wako wa kipekee)
5. Jinsi Ya Kufanikiwa Katikati Ya Nyakati Ngumu.
6. Saikolojia Ya Mteja
7. Mbinu Za Kujenga Ujasiri Na Kujiamini.
8. Surviving The Crisis.

TEMBELEA MITANDANO YA KIJAMII YA JOEL NANAUKA

YouTube: **Joel Nanaka**

(Utapata VIDEO nyingi za kukufundisha mambo mbalimbali)

Instagram: **JoelNanauka_**

(Utapata mafunzo kila siku yatakayokusaidia)

Facebook: **JNanauka**

(Utapata mafunzo kila siku na pia shuhuda mbalimbali.)

Kupata vitabu vingine vilivyoandikwa na **Joel Nanauka** wasiliana na namba zifuatazo:

0745 252 670

0756 094 875

0683 052 686